



MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

TAARIFA FUPI YA USHIRIKI WA VETA
KWENYE MAONESHO YA SABASABA
NA NANENANE 2018

**MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI
STADI
(VETA)**



... i ...

TAARIFA FUPI YA USHIRIKI WA VETA KWENYE MAONESHO YA SABASABA NA NANENANE 2018

Juni –Agosti 2018

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imekuwa ikishiriki kwenye maonesho ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam pamoja na maonesho ya Wakulima yanayofanyika nchini kila mwaka kwa lengo la kutangaza na kueneza shughuli zake.

Umuhimu wa maonesho hayo ni;

- Sehemu inayowezesha kuwafikia watu wengi moja kwa moja katika kuwafahamisha shughuli na huduma za mamlaka, hivyo kutambulika na kukubalika zaidi;
- Huwezesha kupata mrejesho wa moja kwa moja kutoka kwa watu wengi juu ya huduma zetu: Maoni, ushauri na mapendelekezo;
- Huwezesha kuonesha umahiri na ubunifu katika ufundi stadi kwa waajiri, wazazi na jamii yote kwa ujumla;
- Huwezesha jamii ya ndani na kimataifa kufahamu vyema shughuli zetu na hivyo kuanzisha ushirikiano (partnership);
- Hutoa fursa kwa walimu na vijana wetu kujifunza teknolojia mbalimbali kutoka kwa washiriki wengine.

1. Maonesho ya 41 ya Biashara ya kimataifa Dar es salaam (Sabasaba)

Maonesho hayo yalianza rasmi tarehe Juni 28 hadi Julai 13 katika viwanja vya Mwl Julius Nyerere barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Mgeni rasmi

Mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonesho alikuwa Raís wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt John Pombe Magufuli .

Kauli mbiu

Kauli mbiu ya maonesho "UKUZAJI WA BIASHARA KWA MAENDELEO YA VIWANDA".

Ujumbe wa VETA "VIWANDA VINAHITAJI UJUZI, UJUZI UNAPATIKANA VETA"

Ushiriki wa VETA

VETA ilikuwa na jumla ya washiriki 73 kutoka katika vyuo mbalimbali nchini vinavyomilikiwa na VETA na visiviyomilikiwa na VETA



Mwenyekiti wa Bodi ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Peter Maduki akipokea tuzo ya Ushindi kutoka kwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Kassim Majaliwa baada ya VETA kuibuka mshindi katika kundi la Uendelezaji Ujuzi na Mafunzo katika maonesho ya Sabasaba mwaka 2018.

Ujuzi na maeneo yaliyooneshwa

VETA ilijikita kuonesha namna Elimu na Mafunzo ya Ufundisti inavyochangia katika kuzalisha nguvukazi yenye ujuzi na ubunifu katika Sekta za Kipaumbele katika Ukuaji wa Uchumi. Maeneo yaliyoguswa ni pamoja na:

Sekta/Eneo	Mambo yaliyooneshwa
UKUZAJI UJUZI KATIKA SEKTA YA MADINI NA UJENZI	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Simulator kwa ajili ya kufundishia ufundi wa mitambo mikubwa-Chuo cha VETA Mwanza; ▪ Taarifa kuhusu mafunzo ya ufundi wa mitambo mikubwa-Chuo cha VETA Shinyanga; ▪ Programu ya Mafunzo ya Ufundisti kwa kushirikiana na Makampuni ya Madini (IMTT)-Chuo cha VETA Moshi ▪ Mafunzo ya Ukataji na Ung'arishaji madini-VETA Shinyanga
UKUZAJI UJUZI KATIKA SEKTA YA UJENZI	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Mafunzo ya Ujenzi wa Barabara-Chuo cha VETA Dodoma; ▪ Mafunzo ya Uchoraji Ramani za majumba-VETA Dsm
UKUZAJI UBUNIFU KWA MAENDELEO YA VIWANDA	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Ubunifu mbalimbali wa kielektroniki kutoka vyuo vya VETA Arusha, Al-Makhtoum, VETA Dar es Salaam na VETA Kipawa;



Wananchi wakipata mafunzo na taarifa mbalimbali katika darasa lililo andaliwa na VETA Kwa ajili ya kufundishia wananchi wakati wa maonesho ya sabasaba mwaka 2018.

UKUZAJI UJUZI KATIKA SEKTA YA NGUO NA MAVAZI	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Ufumaji (Handloom weaving-VETA Tabora) ▪ Kudarizi kwa kutumia kompyuta-VETA Lindi ▪ Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi-VETA Dakawa ▪ Utengenezaji batiki na vifaa vyaa maabara-VETA Dsm
UKUZAJI UJUZI KWA AJILI YA SEKTA YA KILIMO	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Ufugaji wa Nyuki Kisasa -VETA Dakawa ▪ Ubunifu wa mashine mbalimbali za kuvuna na kuchakata mazao (kutoka kupukuchua mahindi kusaga nafaka, na kukoboa VETA Mbeya; kusaga karanga na juisi kutoka VETA Moshi; ▪ Mashine ya kukaushia mazao -VETA Songea ▪ Pampu mbalimbali kutoka VETA Moshi ▪ Mashine ya kuchomelea kwa kutumia chumvi- VETA Mara; ▪ Bustani wima yenyewe mfumo wa umwagiliaji -VETA Kihonda ▪ Mfumo wa kunawa mikono unaoendeshwa kwa mguu ▪ Mfumo wa kufukuza ndege mashambani -VETA Mikumi ▪ Mashine ya kunyonyizia dawa mashambani – VETA Mikumi ▪ Majiko makubwa ya umeme na gesi – VETA Moshi
UKUZAJI UJUZI KATIKA SEKTA YA UTALII	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Mafunzo ya Utalii wa kiutamaduni-VETA Mikumi
USHIRIKIANO NA WADAU KATIKA MAFUNZO	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Ushirikiano na Airtel katika mafunzo kwa njia ya Simu-VSOMO ▪ Ushirikiano na VSO na Makampuni ya Gesi katika Mafunzo ya Ufundsi Stadi kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara



Wafanyakazi pamoja na Wanafunzi wa VETA wakiwa katika nyuso za furaha wakishangilia ushindi walio upata mara baada ya VETA Kuibuka mshindi wa kwanza katika kundi kundi la Uendelezaji Ujuzi na Mafunzo Mafunzo wakati wa maonesho ya sabasaba mwaka 2018.



Viongozi walio tembelea banda la VETA Katika maonesho ya Sabasaba mwaka 2018.

U T U N Z A J I MAZINGIRA KWA MAENDELEO YA VIWANDA	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Ubunifu wa bidhaa mbalimbali kwa kutumia vumbi la mbao. ▪ Utengenezaji meza na stuli kwa kutumia mifuniko ya chupa za plastiki-mhitimu wa ufundi stadi asiyeona
UBUNIFU WA BIDHAA MBALIM- BALI	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Ubunifu wa kielekroniki na kidigitali ▪ Smart house ▪ Kengele inayojiendesha ▪ Mfumo unaomlazimisha dereva wa pipipiki kuvala kofia ngumu (helmet) wakati wote anapoendesha; ▪ Mfumo wa kupiga kengele unaojiendesha; ▪ Mfumo wa kubembeleza watoto kulala na kuwaamsha; ▪ Mfumo wa kuoshea magari unaojiendesha ▪ Mfumo wa kufukuza ndege waharibifu mashambani ▪ Mfumo wa kuzuia mota za "three phase" kuungua; ▪ Mashine za kuchanganya juisi na kusagia juice
DARASA LA MAO- NESHO (DARASA LA VETA SABASA- BA)	VETA iliendesha darasa halisi la mfano kwa wananchi walitembelea maonesho hayo ambapo wananchi walikuwa na fursa ya kukaa na kufuatilia mafunzo mbalimba-li bila malipo. Darasa hilo lilitoa mafunzo ya aina mbali mbali kama vile ufgaji wa kuku, ufgaji wa nyuki, upambaji, Udereva na Mapishi.

Mafanikio

- Jumla ya watu 59,101 wakiwemo wageni mashuhuri 19 walitembelea banda la VETA. Kati yao 58,788 (96%) walisema maonesho ya huduma zetu ni mazuri sana, 2207 (3.7) mazuri na 324 (0.54%) wastani.

- VETA iliibuka mshindi wa kwanza kwenye kundi la Uendelezaji mafunzo na kupewa tuzo.
- Kuongezeka kwa elimu na uelewa wa umma juu ya majukumu na kazi za VETA na maswala ya VET.
- VETA imeweza kufuta shaka kwa watu kuhusu ufahamu wao wa VETA na inafanya kazi.
- VETA ilikuwa na fursa ya kuonyesha uvumbuzi wake kwa umma na kwa waajiri.
- VETA pia ilipata nafasi ya kupata mawazo mapya na ujuzi kwa njia ya ushauri uliotolewa na watu (wageni) ambao wanatembelea.
- VETA ilipata nafasi ya kutangazwa katika vyombo vyaa habari

2. Maonesho ya Wakulima (Nanenane)

Maonesho hayo yalifanyika kuanzia Agosti 1 hadi 9, 2018 katika viwanja vya Nyakibindi wilayani Bariadi mkoani Simiyu.



Wananchi mbalimbali walio tembelea banda la VETA wakati wa maonesho ya Nanenane wakipata taarifa kuhusiana na mafunzo yanayo husiana na kilimo na Ufugaji yanayo tolewa na VETA katika vyuo vyake, wakati wa maonesho ya Nanenane yaliyofanyika kitaifa Mkoani Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi Wilayani Bariadi.



Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Magharibi ndugu Wilhard Soko akipokea tuzo kutoka kwa Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa baada ya VETA kuibuka mshindi wa kwanza kwenye kundi la Vyuo vinavyotoa Mafunzo katika Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika kitaifa Mkoani Simiyu Wilayani Bariadi.



Wafanyakazi pamoja na Wanafunzi wa VETA wakiwa katika nyuso za furaha wakishangilia ushindi walio upata mara baada ya VETA Kuibuka mshindi wa kwanza katika kundi kundi la vyuo vinavyo toa mafunzo.

Mgeni rasmi

Maonesho ya Nanenane yalifunguliwa rasmi na aliyekuwa Waziri wa Kilimo Dkt Charles Tizeba na kufungwa na Rais mstaafu wa awamu ya tatu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.



Aliye kuwa Waziri Wa Kilimo,Mifugo na Uvuvi Dkt.Charles John Tizeba akipata taarifa mbalimbali alipotembelea banda la VETA wakati wa maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa Mkoani Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi Wilayani Bariadi.

Kauli Mbiu

Wekeza kwenye Kilimo, Ufugaji na Uvuvi kwa maendeleo ya Viwanda.

Washiriki

VETA ilikuwa na jumla ya washiriki 25 kutoka katika vyuo mbalimbali vyua ufundsi stadi nchini.

Ujuzi na maeneo yaliyooneshwa

VETA ilioneshaa mafunzo yanayotolewa katika vyuo vyake yanayoendana na kilimo, teknolojia na ubunifu uliofanywa na walimu na wanafunzi katika vyuo mbalimbali. Mafunzo, teknolojia na ubunifu uliooneshwa ni pamoja na mafunzo ya ufugaji wa kuku, bidhaa za ngozi, ufugaji wa nyuki, ufundsi wa zana za kilimo, heavy duty equipment mechanics; ukataji na ung`arishaji vito, ubunifu wa vifaa vyua umwagiliaji (sprinkler), dawati linaloweza kutumika kwa matumizi mengi, kifaa cha kufukuza ndege waharibifu mashambani na bidhaa zinazozalishwa kutokana na Maranda ya mbao.

Pia taarifa mbalimbali za mafunzo na soko la ajira zilitolewa kwa watu waliotembelea banda la VETA pamoja na utoaji wa fomu za kujiunga na elimu na mafunzo ya ufundsi stadi.

Darasa maalum pia lilikuwepo ambapo mada mbalimbali zilitolewa kwa siku zote za maonesho bila gharama yoyote.



Baadhi ya Wananchi walio tembelea banda la VETA wakati wa maonesho ya Nanenane

Mafanikio

- Jumlayawatu 40,608 walitembelea banda la VETA katika maonesho hayo ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo maonesho hayo yalifanyika mkoani Lindi na idadi ya watembeleaji ilikuwa ni 2,500.
- **VETA** iliibuka mshindi katika kundi la taasisi za utoaji mafunzo.
- Wadau mbalimbali walijitokeza kutaka kuanzisha ushirikiano na kusaidia uendeshaji wa shughuli za mafunzo. Wadau hao ni pamoja na :
 - i. **TIRDO – Utoaji mafunzo ya bidhaa za ngozi kupitia mradi wa Dual apprenticeship training :** Mwakilishi wa TIRDO Dkt. Shadrack Kangonde (simu 0756547638) aliitembelea banda la VETA wakati wa maonesho na kutoa wazo la ushirikiano kati ya TIRDO, LAPF na Magereza kupitia kiwanda chake cha kuchakata ngozi cha Karanga mkoani Kilimanjaro kutoa mafunzo ya bidhaa za ngozi kwa vijana kupitia mfumo wa uwaganenzi;
 - ii. **Mfuko wa Rais wa kujitegemea** (Presidential Trust for Self-Reliance – Mwakilishi wa taasisi hiyo Ndg. Kessy (simu. 0754773642) aliwasilisha wazo la kuwasaidia wahitimu wa ufundi stadi kwa kuwapatia vifaa/mikopo ya kuwawezesha kujajiri. Alipendekeza uhamasishaji ufanyike katika wilaya mbalimbali ili vijana hao wajitokeze na kupatiwa mikopo.

Maswa na kusafiri kila siku kwenda Bariadi.
Hali hii ilisababisha uchovu kwa washiriki na
kuongeza ghamama za mafuta.

Changamoto zilizojitokeza kutoka kwa wananchi

- ❖ Uelewa mdogo wa umma kuhusu VETA: Wengi wa watu wanajua kuwepo kwa VETA, lakini hawajui majukumu yake.
- ❖ Uelewa mdogo wa umma juu ya kozi zinazotolewa na VETA: Watu wengi hawajui kozi tofauti tofauti zinazotolewa na VETA.
- ❖ Maswali mengi kuhusu ujenzi wa Chuo cha VETA Simiyu ambapo wananchi wengi ikiwemo viongozi walitembelea banda la VETA walitaka kufahamu ujenzi wa chuo hicho umefika katika hatua gani.

MAPENDEKEZO

- Fedha za maandalizi ya vifaa vyta maonesho zipatikane mapema kwenye vituo
- Mamlaka iwe inatenga fedha za tahadhari katika kipindi cha maonesho ili kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya muda ambayo yanaweza kujitokeza kama ilivyotokea mwaka 2017.
- Baadhi ya vifaa vilivyooneshwa viboreshwe ili mwakani virudishwe katika maonesho
- Mamlaka itenge sehemu maalumu (show room) kwaajili ya kuweka bidhaa zilizobuniwa kutoka vyuo mbalimbali vyta VETA.

- iii. **Baraza la Taifa la Uwezeshaji (NEEC)**- utoaji mafunzo kwa watu wenye ulemavu. Afisa wa NEEC Ndg. Nyakaho (simu. 0655884148) alijulisha VETA kuwa ina mawasiliano na taasisi ziziso za kiserikali nchini Afrika Kusini ambapo taasisi hizo zimeonesha nia ya kuwasaidia wenye ulemavu kwa kuwapatia mafunzo ya Ufundı Stadi. Aliomba VETA kufanya mawasiliano na NEEC ili kuandaa andiko.
- iv. Wizara ya Kilimo – Msaada wa vitabu vya kufundishia ufundi wa zana za kilimo. Wawakilishi wa Wizara hiyo waliotembelea banda la VETA walitoa taarifa ya uwepo wa vitabu vitakavyofaa kufundishia fani hiyo na kuitaka VETA kuandika barua rasmi ya kuomba kupatiwa vitabu hivyo.

Changamoto zilizojitokeza kwenye maonesho hayo ni:

- Hapakuwa na muda wa kutosha kufanya maandalizi ya vifaa vya maonesho (zimamoto) kwa kanda ya Dsm;
- Bajeti ya kufanya maandalizi ya vifaa vya maonesho;
- Muda wa maonesho uliongezwa na hivyo kuathiri utendaji hata kupelekea kupunguzwa kwa baadhi ya washiriki.Kwa Sabasaba muda uliongezwa kwa siku tano na kwa Nanenane siku zilizoongezwa ni tatu.
- Ukosefu wa Malazi kwa washiriki walioenda kwenye maonesho ya Nanenane mkoani Simiyu ambapo ilibidi washiriki walale wilaya ya



Baadhi ya Wananchi walio tembelea banda la VETA wakati wa maonesho ya Nanenane



PREPARED BY:
VETA P.O.BOX 2849 DAR ES SALAAM
Printing At Dar es Salaam Rvtsc - Printing School